# 坦桑尼亚联合共和国

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## 教育科技部

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA


坦桑尼亚联合共和国
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
教育科技部
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

许可证
Cheti cha Ithibati

编号 Na. 1096

大纲名称：小学汉语教学大纲
Jina la Chapisho: Muhtasari wa Lugha ya Kichina Elimu ya Msingi Darasa la III - VI

出版机构：坦桑尼亚教育学院
Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

作者：教育科技部
Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-844-6

此教学大纲已于 2023 年6月29号 由坦桑尼亚教育科技部批准，作为坦桑尼亚小学汉语教学大纲。

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Lugha ya Kichina Elimu ya Msingi Darasa la III - VI Tanzania Bara.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa 博士
Kamishna wa Elimu 教育专员

# 小学汉语教学大纲

# MUHTASARI WA LUGHA YA KICHINA ELIMU YA MSINGI

## 小学三至六年级

## DARASA LA III–VI

**2023年**

© 坦桑尼亚教育学院 2023年
2023 年第一版
书号: 978-9987-09-844-6

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023
Toleo la Kwanza 2023
ISBN: 978-9987-09-844-6

坦桑尼亚教育学院
Mikocheni地区
Ali Hassan Mwinyi 路132 好
邮编35094
14112 达累斯萨拉姆

电话 +255 735 041 168/735 041 170
电子邮箱：director.general@tie.go.tz
网址: www.tie.go.tz

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168/735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

引用本大纲请注明来源：坦桑尼亚教育科技部（2023年）。小学三至六年级汉语课程大纲。坦桑尼亚教育学院。

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). Muhtasari wa Lugha ya Kichina Elimu ya Msingi Darasa la III-VI. Taasisi ya Elimu Tanzania.

版权所有。未经坦桑尼亚教育学院书面许可，不得以任何形式复制、出版、翻译或提供本大纲。

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Tasisi ya Elimu Tanzania.

# 目录 Yaliyomo


表目录Orodha ya Majedwali ..... v

缩写Vifupisho ..... vi

致谢Shukurani ..... vii

1.0 简介Utangulizi ..... 1

2.0 坦桑尼亚教育的总目标 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ..... 1

3.0 小学三至六年级阶段教育目标Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI ..... 2

4.0 小学三至六年级的综合教育能力Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III-VI ..... 4

5.0 小学三年级至六年级的主要能力和具体能力Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ..... 5

6.0 教师、学生和家长/监护人在教学中的作用Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 6

6.1 教师Mwalimu ..... 6

6.2 学生Mwanafunzi ..... 8

6.3 家长/监护人Mzazi/Mlezi ..... 8

7.0 建议的教学方法 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 9

8.0 教学资源/材料 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 9

9.0 在教学中的评估Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 10

10.0 课时数量Idadi ya Vipindi ..... 11
11.0 大纲内容Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 11
三年级Darasa la III ..... 12
四年级Darasa la IV ..... 30
五年级Darasa la V ..... 44
六年级Darasa la VI ..... 59
参考目录 Bibliografia ..... 71

# 表目录 **Orodha ya Majedwali**


表**1: Jedwali 1:** 三至六年级的主要能力和具体能力Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la III-VI .................. 5

表**2: Jedwali 2:** 三年级的具体内容 Maudhui ya Darasa la III .................................................................................... 12

表**3: Jedwali 3:** 四年级的具体内容 Maudhui ya Darasa la IV .................................................................................... 30

表**4: Jedwali 4:**五年级的具体内容 Maudhui ya Darasa la V ....................................................................................... 44

表**5: Jedwali 5:** 六年级的具体内容 Maudhui ya Darasa la VI .................................................................................... 59

## 缩写 **Vifupisho**

| | |
|---|---|
| **TET** | 坦桑尼亚教育研究所 Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **LAT** | 坦桑尼亚手语 Lugha ya Alama ya Tanzania |
| **TEHAMA** | 信息与通信技术 Teknolojia ya Habari na Mawasiliaono |

## 致谢**Shukurani**

小学三至六年级汉语课程大纲的准备涉及了来自政府和非政府机构的各类专家。坦桑尼亚教育研究所（TIE）承认并感激所有为该大纲的制定做出贡献的参与者。此外，TIE特别感谢讲师、培训师、学校质量控制员、教师以及TIE课程开发人员。此外，TIE衷心感谢由教育、科学和技术部任命的幼儿园、小学、中学和师范教育课程改进任务的全国专家委员会。该委员会以专业的态度确保该大纲的内容旨在培养具备知识、技能和态度的毕业生，使他们能够自谋职业、就业并维持日常生活，这是2023年课程改进的主要目标。

最后，TIE对教育、科学和技术部为该大纲的准备和分发提供便利表示特别的感激之情。

Maandalizi ya Muhtasari wa Lugha ya Kichina Elimu ya Msingi Darasa la III–VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu, pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Uboreshaji wa Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la Uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Aneth A. Komba博士
总监
坦桑尼亚教育学院

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 简介**Utangulizi**

中文是从三年级到六年级的小学阶段的选修课程。该课程旨在培养学生在听、说、读、写方面的中文能力，并使他们能够根据不同情境中的交流需求轻松运用该语言。中文能够促进投资和商业活动中的重要合作，从而促进经济发展。中文语言开启了各种机会，包括自主就业和就业。

这份教学大纲旨在指导坦桑尼亚大陆三年级到六年级小学教师进行中文教学。该大纲是对2023年小学教育课程的翻译。此外，该大纲将使教师能够通过培养学生在调查、创造力、合作、沟通和问题解决方面的能力来规划教学活动，适应他们所处的环境。

Lugha ya Kichina ni somo chaguzi katika ngazi ya Elimu ya Msingi kuanzia Darasa la III-VI. Somo hili linalenga kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika kwa Lugha ya Kichina, na kumjengea uwezo wa kutumia lugha hiyo kwa urahisi kulingana na mahitaji ya mawasiliano katika miktadha mbalimbali. Lugha hii inasaidia kukuza ushirikiano katika uwekezaji na shughuli za kibiashara, hivyo kuchangia maendeleo ya kiuchumi. Lugha ya Kichina inafungua fursa mbalimbali zikiwemo za kujiajiri na kuajiriwa.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lugha ya Kichina Elimu ya Msingi, Darasa la III-VI Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Aidha, Muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake.

## 2.0 坦桑尼亚教育的总目标 **Malengo Makuu ya Elimu Tanzania**

坦桑尼亚教育的主要目标是使每个坦桑尼亚人能够：Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) 提升和改善个人品格，培养自尊和自信心； Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) 尊重坦桑尼亚的文化、传统和习俗，以及不同的文化观点、人道主义、人权和包容态度与行动；Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) 学习知识并运用科学技术进行创新，培养批判性思维、创造力、合作沟通和积极的人生态度，在个人发展以及国家和整个世界的可持续发展中发挥作用；Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) 理解并保护国家的核心价值观，包括人性、爱国主义、正直、团结、真诚、诚实、责任心和国家语言；Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) 培养生活技能和就业技能，提高日常生活的效率；Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) 倡导以爱和尊重为基础的职业道德，以提高生产和服务提供的生产力和效率；Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) 认识和解决跨领域问题，包括人们（社会）的健康和福祉、性别平等，以及环境的可持续发展和保护；Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira.

(h) 促进国家和国际合作、和平与正义，遵守国家宪法和国际协议。Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 小学三至六年级阶段教育目标 **Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI**

小学三至六年级的阶段教育目标是使学生能够：Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la Tatu hadi la Sita ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) 掌握流利的语言、坦桑尼亚手语 (LAT) 和阅读、写作、计算能力和沟通能力；Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;

(b) 理解、使用和珍视斯瓦希里语和英语。此外，根据学校的实际情况，鼓励学生至少掌握一种外语；Kufahamu, kutumia na kuthamini lugha za Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni;

(c) 珍视和传承坦桑尼亚的文化，维护国家团结，并认识其他文化；Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) 学习知识、培养探究能力、逻辑思维、创新和解决问题的能力；Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) 培养道德品质、诚信和尊重信仰的差异；Kukuza maadili, uadilifu, na kuheshimu tofauti za imani;

(f) 发现天赋和培养才艺、职业、体育和艺术技能；Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;

(g) 培养珍视和热爱工作的态度；Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) 在学习和日常生活中认识和应用科学和技术；Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na katika maisha ya kila siku;

(i) 学习环境保护、性别平等和其他综合问题的知识、培养相关技能和意识；Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) 提高在包容性环境中相互交往的能力。Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 4.0 小学三至六年级的综合教育能力**Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III-VI**

三至六年级学生将培养的综合教育能力是
Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la III – VI ni:

(a) 流利地使用坦桑尼亚手语（LAT）和手语的阅读、写作、计数和交流；Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;

(b) 使用和欣赏斯瓦希里语、汉语和至少一种其他外语；Kutumia na kuithamini lugha ya Kiswahili, Kiingereza, na angalau lugha nyingine moja ya kigeni；

(c) 展示、欣赏和尊重坦桑尼亚文化和民族团结，承认其他文化；Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) 探究、求实、设计和解决问题；Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) 表现出正直并尊重不同的信仰。Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za Imani;

(f) 在各种情况下合理使用才能、天赋、工作技能、体育和艺术技巧；Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali;

(g) 欣赏和热爱工作；Kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) 在学习和日常生活中使用科学技术；Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;

(i) 保护环境，尊重性别平等和其他跨领域问题；Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) 在包容的环境中进行社交。Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 5. 0 小学三年级至六年级的主要能力和具体能力**Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi**

小学汉语教学大纲所指的主要能力和具体能力，如表1所示。Muhtasari wa Lugha ya Kichina Elimu ya msingi kwa Darasa la III-VI una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama unavyobainishwa katika Jedwali Na 1.

表**1: Jedwali 1:** 三至六年级的主要能力和具体能力*Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Darasa la III-VI*

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** |
|---|---|
| 1.0 掌握基本汉语技能<br>Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kichina | 1.1 培养汉语声母、韵母、声调的音素意识并掌握发音和汉字<br>Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya awali, mwisho, toni na hanzi<br>1.2 能够联系字词与环境中的对象<br>Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira<br>1.3 掌握简单的语法和词汇<br>Kumudu sarufi na msamiati sahili |
| 2.0 在对话和写作中展示对信息的理解<br>Kuonesha uelewa wa taarifa katika mazunguzo na maandishi | 2.1 听懂表达的内容<br>Kusikiliza na kuelewa taarifa<br>2.2 阅读和理解简单的文本<br>Kusoma na kuelewa matini sahili<br>2.3 在熟悉的对话环境中做出正确回应<br>Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika<br>2.4 阅读简单的文本<br>Kusoma matini sahili |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** |
|---|---|
| 3.0 在不同的语境下进行有效交流<br>Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali | 3.1 展现对口语和书面语言基本特征的理解<br>Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi<br>3.2 使用适当的语法和词汇在各种环境中简单交流<br>Kuzungumza katika miktadha mbalimbali kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka<br>3.3 在不同的语境中，使用适当的语法和词汇进行书面交流<br>Kuwasiliana kwa maandishi katika miktadha mbalimbali kwa kutumia sarufi na msamiati mwafaka |

## 6. 0 教师、学生和家长/监护人在教学中的作用**Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji**

教学和学习依赖于教师、学生和家长之间的紧密合作来完成各种任务。这些任务包括：Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu hayo ni kama yafuatayo:

### 6. 1 教师**Mwalimu**

教师应该：Mwalimu anatarajiwa:

（a） 使学生在斯瓦希里语课程中学习并达到预期的熟练程度；Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika lugha ya Kichina;

（b） 根据学生的年龄、特殊需求和能力使用恰当的教学和学习方法，使学生能够：Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, na mahitaji anuai zitakazomwezesha mwanafunzi:

(i) 培养 21 世纪所需的能力；及Kujenga umahiri unohitajika katika Karne ya 21; na

(ii) 全面参与教学和学习过程；Kushiriki kikamilifu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(c) 使用包括帮助学生思考、反思和从不同来源获取知识的协作方法，使学生成为学习的核心。推荐的教学和学习方法包括实践工作、研究、科学实验、讨论和问题解决，以解决学生现实环境中的问题。此外，鼓励教师根据教学文本使用其他类似方法以实现预期的能力构建；Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;

(d) 创设一个安全的教学和学习环境的课堂；Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) 制作和选择教学和学习工具；Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) 通过使用各种测量和评估工具和方法进行定期的持续评估，包括谜题、清单审核、实验、问卷调查、面对面提问、练习、实践工作（个人工作和小组工作）、问题解决和作业包。其他工具和方法包括实践实验、演讲、学期考试和期末考试；Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki,majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;

(g) 确保学习和教学活动对每个学生都公正和平等，不受其差异的影响；Kuhakikisha kuwa ujifunzaji na ufundishaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) 在学校保护学生的安全；Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) 监测学生的日常进展；Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) 确定学生的需求并提供适当的支持；Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) 将家长/监护人和社区参与学生学习的各个阶段；和Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) 在教学和学习中整合综合问题和信息技术。Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

## 6. 2 学生**Mwanafunzi**

学生应该：Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) 成为学习过程中的主要执行者；
Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) 参与各种课内外学习活动，以达到预期的能力；和Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na

(c) 从不同来源（包括教科书、其他出版物和在线图书馆）中寻求知识。Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao.

## 6. 3 家长/监护人**Mzazi/Mlezi**

我们期望家长/监护人能够：Mzazi/ Mlezi anatarajiwa:

(a) 监督和追踪孩子的学习进展；Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) 在可能的情况下管理孩子完成他们的学术任务；Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) 确保家庭环境友好和安全，促进学习；Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(d) 监控孩子的行为表现；Kufuatilia mwenendo wa kitabia wa mtoto;

(e) 为孩子提供所需的学习工具；Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika shughuli ya ujifunzaji;

(f) 确保学生获得基本需求；和 Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na

(g) 教育孩子教育和工作的重要性和价值，并鼓励他们努力学习。Kumfundisha mtoto umuhimu na thamani ya elimu na kazi pamoja na kumuhimiza kujifunza kwa bidii.

## 7. 0 建议的教学方法 **Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

教学方法对于培养学生的能力至关重要。本教学大纲为每个活动提供了教学和学习方法的建议。其中包括实地考察、小组合作和实践任务等方法。然而，建议教师根据教学和学习的具体情境使用其他类似的方法。

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazimradi na kazi za vitendo. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 8. 0 教学资源/材料 **Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji**

教学过程需要各种工具/设备来培养所期望的能力。因此，教师和学生在需要时应当合作准备或选择学校和家中可用的替代工具/设备。教师和学生应当从各种来源寻求信息，以提高教学和学习过程的有效性。一份经过批准的参考资料清单将由坦桑尼亚教育研究所（TET）提供。

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana mbadala zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi vinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

## 9.0 在教学中的评估**Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji**

评估是促进所期望的能力建设的教学和学习过程中的重要问题。汉语科目的评估将包括持续评估和期末评估。持续评估将关注学习活动中规定的标准，并使教师能够确定学生在学习中的能力和需求。此外，它还将评估学生在周围环境中运用所学技能、评价、叙述和应用的变化。教师将使用评估信息来改进教学，并帮助学生达到学习目标。在教学和学习过程中可以使用的评估工具包括思维导图、检查清单、课堂练习、实验、实践实验、问卷调查、面对面问题、练习、实践工作（个人和小组作业）、随机作业、作品集和其他类似工具。期末评估将涉及每周、每学期和年度末的考试，用于评估学生的学习进展。这些评估信息将用于评估学生的发展，并提供反馈以促进教学和学习。此外，还将进行小学六年级的全国性评估，该评估将为高中四年级的考试提供7.5分。Upimaji ni suala muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa lugha ya Kichina utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo.

Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathimini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, kutakuwa na upimaji wa kitaifa wa Darasa la Sita ambao utachangia alama 7.5 katika mtihani wa Kidato cha Nne.

## 10.0 课时数量 **Idadi ya Vipindi**

小学汉语教学大纲提供了教学所需的时间估计，考虑到具体能力的复杂性和学生需要完成的活动，时间估计以40分钟为单位。因此，对于三年级至六年级的学生，每周安排了两个课时来进行汉语学习。

Muhtasari wa lugha ya Kichina Elimu ya Msingi Darasa la III - VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni viwili (2) kwa wiki kwa Darasa la III - VI.

## 11.0 大纲内容Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

大纲内容排列在一个表格中，其中包含七个列：主要能力、具体能力、学习活动、建议的教学方法、评估标准，教学资源和课时数量如表1所示2-5。Maudhui ya muhtasari huu yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele saba ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu pendekezwa, vigezo vya upimaji, zana/vifaa pamoja na idadi ya vipindi kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2–5.

# 三年级 **Darasa la III**

表2：**Jedwali 2:** 三年级的具体内容*Maudhui ya Darasa la III*

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 掌握基本汉语技能<br>Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kichina | 1.1 掌握汉语声母、韵母和声调的音素意识和发音以及汉字<br>Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya awali, mwisho, toni na hanzi | (a) 听并发音汉语声母<br>Kusikiliza na kutamka konsonanti za kichina | 听后模仿：引导学生流利地发音汉语声母（如b、p、m、f、d、t、l）<br>**Kusikiliza na kuiga :** Ongoza wanafunzi kutamka kwa ufasaha konsonanti za kichina kwa sauti kubwa (mfano: b, p, m, f, d, t, l)<br>边唱边发音：边唱边引导学生发声母，享受声母的发音<br>**Kutamka kwa kuimba:** Ongoza wanafunzi kutamka konsonanti za kichina huku wakiwa wanaziimba na kufurahia utamkaji wa konsonanti hizo | 汉语声母被听到并发音<br>Konsonanti za kichina zimesikilizwa na kutamkwa | 声母卡、字母卡、音频成绩单、电影、田字格<br>Kadi zenye Konsonanti, kadi zenye irabu，Nakala za sauti, picha mwendo, tianzige | 24 |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量 **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 数字化方法：引导学生在音频设备（如CD、扬声器或电视）上听声母 **Midia**：Ongoza wanafunzi kusikiliza konsonanti kwenye vinasasauti (mfano: CD, spika au televisheni) | | | |
| | | (b) 读和写汉语声母 Kusoma na kuandika konsonanti za kichina | 使用声母卡片：引导学生流利地读出展示给他们的卡片（读出卡片上的声母并写出那个声母，每个声母最好写5次以上）**Kutumia kadi za konsonanti**: Ongoza wanafunzi kusoma kwa ufasaha kadi anazoonyeshwa (asome konsonanti iliyopo kwenye kadi na kuiandika konsonanti hiyo, ni vyema kila konsonanti ikaandikwa zaidi ya mara 5) | 汉语声母被流利阅读和书写了 Konsonanti za kichina zimesomwa na kuandikwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 游戏：引导学生找出隐藏的声母卡片，找到卡片的人读并写（被同学表扬）<br>**Michezo:** Ongoza wanafunzi kutafuta kadi za konsonanti zilizofichwa, atakayepata kadi asome na kuiandika( apongezwe na wanafunzi wenzake)<br><br>竞赛：带领学生比拼阅读声母流畅度和拼写<br>**Mashindano:** Ongoza wanafunzi kushindana kusoma konsonanti kwa ufasaha na kuandika konsonanti | | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) 听和发音基本的韵母<br>Kusikiliza na kutamka irabu za msingi za kichina | 聆听和跟读:指导学生认真聆听老师或者电子设备发出的韵母并正确跟读<br>**Kusikiliza na kurudia:** Ongoza wanafunzi kusikiliza sauti ya mwalimu au nakala za sauti na kurudia kwa ufasaha kutamka irabu walizosikia<br>听唱：引导学生流利听唱韵母歌（每人唱一首韵母歌）<br>**Kusikiliza na kuimba:** Ongoza wanafunzi kusikiliza na kuimba irabu kwa ufasaha(kila mwanafunzi aimbe wimbo wa irabu) | 韵母被听到并流利地发<br>Irabu za kichina zimetamkwa na kusikilizwa | | |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) 读写基本的韵母 Kusoma na kuandika irabu za msingi za kichina | 使用韵母卡：引导学生流利地阅读展示给他们的卡片（读卡上的韵母并写韵母，每个声母最好写5次以上）<br>**Kutumia kadi za irabu**: Ongoza wanafunzi kusoma kwa ufasaha kadi anazoonyeshwa (asome irabu iliyopo kwenye kadi na kuiandika irabu hiyo, ni vyema kila konsonanti ikaandikwa zaidi ya mara 5)<br>游戏：引导学生找到隐藏的字母卡片，找到卡片的人要读和写（被同学表扬）<br>**Michezo:** Ongoza wanafunzi kutafuta kadi za irabu zilizofichwa, atakayepata kadi asome na kuiandika | 韵母被读和写 Irabu za kichina zimesomwa na kuandikwa | | |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ( apongezwe na wenzake)<br>比赛：带领学生在阅读流畅度和拼写方面进行比赛**Mashindano:** Ongoza wanafunzi kushindana kwenye kusoma kwa ufasaha na kuandika irabu | | | |
| | | (e) 识别语音和写作中的汉语声调 Kubaini toni za kichina katika matamshi na maandishi | 认真聆听：指导学生认真聆听汉语声调老师朗读学生识别<br>**Kusikiliza:** Ongoza wanafunzi kusikiliza toni za kichina mwalimu kusoma toni hizo huku wanafunzi wakizibainisha<br>朗读：引导学生流利地朗读声调，教师展示声调的动作（上升和下降）并写出声调 | 语音和写作中地汉语声调被识别了<br>Toni za kichina zimebainishwa katika matamshi na maandishi | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kusoma kwa sauti**: Ongoza wanafunzi kusoma toni kwa ufasaha, mwalimu kuonyesha toni kwa vitendo kupanda na kushuka na kuziandika | | | |
| | | (f) 书写一个到两个笔画的汉字<br>Kuandika hanzi za kichina zenye kijenzi kimoja hadi viwili | 听写：指导学生写最多两笔的汉字<br>**Imla :** Ongoza wanafunzi kuandika hanzi za kichina zenye kijenzi kimoja hadi viwili | 一个到两个笔画的汉字被写了<br>Hanzi za kichina zenye kijenzi kimoja hadi viwili zimeandikwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2将环境中的单词和物体联系起来<br>Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira | (a) 识别在教室和学校环境中发现的各种物体的名称<br>Kubaini majina ya vitu mbalimbali vinavyopatikana darasani na katika mazingira ya shule | 即时提问：引导学生针对课堂上发现的各种物品（如黑板、桌子、笔）进行即时提问 **Maswali ya papo kwa papo:** Ongoza wanafunzi kujibu waswali ya papo kwa papo ya vitu mbalimbali vinavyopatikana darasani Mfano: ubao, meza kalamu)<br>设计环境：引导学生设计课堂环境，确定课堂上应该有的东西**Mazingira ya kubuni**: Ongoza wanafunzi kubuni mazingira ya darasa na kubainisha vitu ambavyo vinatakiwa kuwa darasani | 在教室和学校环境中发现的各种事物 的名称都被明确的定义<br>Majina ya vitu mbalimbali vinavyopatikana darasani na katika mazingira ya shule yamebainishwa | 教室图片、 实物字母卡、音频成绩单、电影和田字格<br>Picha ya darasa, vitu halisi, kadi za maneno, nakala za sauti, picha mwendo, kinasa sauti na tianzige | 16 |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) 识别发生在课堂和学校环境中的各种行为<br>Kubaini vitendo mbalimbali vinavyofanyika darasani na katika mazingira ya shule | 看和做：引导学生识别课堂上发生的动作（如坐、站、写、伸手提问等）<br>**Kuona na kutenda:** Ongoza wanafunzi kubaini matendo yanayofanyika darasani (Mfano: kukaa, kusimama , kuandika , kunyoosha mkono kuuliza swali n.k)<br><br>小组：带领学生在小组中比较课堂上发生的不同活动<br>**Makundi madogo madogo:** Ongoza wanafunzi kwenye makundi madogo madogo kubainisha vitendo mbalimbali vinavyofanyika darasani<br><br>表演：带领学生表演课堂上发生的动作，（如教学、提问等）**Maigizo:** | 明确定义了发生在课堂和学校环境中的各种行为<br>Vitendo mbalimbali vinavyofanyika darasani na katika mazingira ya shule vimebainishwa | | |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ongoza wanafunzi kuigiza vitendo vinavyofanyika darasani, (Mfano: kufundisha, kuuliza swali n.k ) | | | |
| | | (c) 读在课堂环境中定义的名称和动作<br>Kusoma majina na vitendo vilivyobainishwa katika mazingira ya darasa | 游戏：通过游戏引导学生读名称，例如寻找藏在教室里的卡片，猜出这些卡片的动作。**Michezo:** Ongoza wanafunzi kusoma majina kwa kutumia michezo kama kutafuta kadi zilizofichwa darasani na kubaini vitendo vya kadi hizo<br>数字法：引导学生使用电视、电脑、计算器来确定课堂上定义的活动<br>**Midia:** Ongoza wanafunzi kutumia televisheni, kompyuta, vishikwambi kubainisha vitendo vinavyobainishwa darasani | 在课堂环境中定义的名称和动作被流利地阅读<br>Majina na vitendo vilivyobainishwa katika mazingira ya darasa vimesomwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) 用拼音写出课堂环境中指定的名称和动作<br>Kuandika majina na vitendo vilivyobainishwa katika mazingira ya darasa | 听写：带领学生写出课堂上规定的名称和动作，（如老师提到动作，学生写出动作名称）<br>**Imla:** Ongoza wanafunzi kuandika majina na vitendo vinavyobainishwa darasani, (Mfano: mwalimu kutaja kitendo na wanafuzi kuandika jina la kitendo hicho) | 课堂环境中指定的名称和动作被流利地用拼音书写了<br>Majina na vitendo vilivyobainishwa katika mazingira ya darasa kuandikwa kwa kutumia pinyin | | |

| 主要能力 Umahiri mkuu | 具体能力 Umahiri mahususi | 学习活动 Shughuli za ujifunzaji | 建议的教学方法 Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | 评估标准 Vigezo vya upimaji | 教学资源 Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | 课时数量 Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 掌握简单的语法和词汇 Kumudu sarufi na msamiati sahili | (a) 用简单的句子介绍自己 Kujitambulisha kwa kutumia sentensi sahili | 游戏：击鼓传花 老师敲鼓学生传递花朵，停止敲鼓花在哪个学生手里他/她就做自我介绍 **Michezo:** Mwalimu apige ngoma wanafunzi wapeane ua mwalimu akiacha kupiga ngoma mwanafunzi mwenye ua atasimama na kujitambulisha | 用简单的句子流利地介绍自己 Sentensi sahili zimetumika katika kujitambulisha | 田字格、电脑、图片和实物 Tianzige, picha, vitu halisi, picha ya watu wakiwa wanatambulishana, na picha ya mtu akiwa anasoma saa vitu halisi | 12 |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) 阅读和书写自我识别中使用的单词<br>Kusoma na kuandika maneno yanayotumika katika kujitambulisha | 朗读课文：学生朗读课文并书写（课文应带有自我识别信息）<br>**Kusoma matini:** wanafunzi kusoma matini na kuandika (matini ibebe ujumbe wa kujitambulisha) | 介绍自己时使用的单词被写了<br>Maneno yanayotumika katika kujitambulisha yamesomwa na kuandikwa | | |
| | | (c) 描述不同的时间（例如早上、下午、晚上）<br>Kubaini nyakati mbalimbali (Mfano: asubuhi, mchana, jioni, n.k) | 图片与描述：引导学生看图片并识别图片的时间<br>**Picha na maelezo:** kuongoza wanafunzi kuangalia picha na kubaini nyakati za picha hizo | 不同的时间被明确的定义<br>Nyakati mbalimbali zimebainishwa | | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 在对话和写作中展示对信息的理解<br>Kuonesha uelewa wa taarifa katika mazungumzo na maandishi | 2.1 在熟悉的对话环境中做出正确回应<br>Kuonesha mwitiko sahihi katika muktadha wa kimawasiliano unaofahamika | (a) 聆听并遵循学校环境中给出的简单指示/说明<br>Kusikiliza na kufuata maagizo/ maelekezo sahili yanayotolewa katika mazingira ya shule | 表演：<br>根据校园主题准备一个短剧表演（老师和学生）<br>**Maigizo:** Andaa igizo fupi linalohusiana na muktadha wa shule (mwalimu na mwanafunzi) | 在学校环境中给出的简单指令/指令被听到并流利地遵循<br>Maagizo/ maelekezo sahili yanayotolewa katika mazingira ya shule yamesikilizwa na kufuatwa | 田字格、图片和实物<br>Tianzige, picha na vitu halisi | 8 |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 在不同的语境下进行有效交流<br>Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali | 3.1 展现对口语和书面语言基本特征的理解<br>Kuonesha uelewa wa sifa za msingi za lugha ya mazungumzo na maandishi | (a) 在简单的交流中使用准确的声调<br>Kutumia toni kwa usahihi katika mawasiliano sahili | 听和理解的练习：使用听和理解的练习，学生需要聆听声音并理解以正确的音调发音的句子的意思。这将帮助他们理解音调对句子意义的影响<br>**Zoezi la kusikiliza na kuelewa:** Tumia mazoezi ya kusikiliza na kuelewa ambapo wanafunzi wanapaswa kusikiliza sauti na kuelewa maana ya sentensi zilizotamkwa kwa toni sahihi | 在简单的交流中使用正确的声调Toni zimetumika kwa usahihi katika mawasiliano sahili | 图片和实物<br>Picha na vitu halisi | 10 |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 自我表达练习：鼓励学生在自我表达时使用正确的音调 您可以给他们提供需要正确音调的常见事物的练习，要求他们使用适当的词语和句子进行表达<br><br>**Mazoezi ya kucheza na kuigiza:** Tumia michezo na mazoezi ya kuigiza kama “kupiga hatua” au “kucheza dansi” ambapo wanafunzi wanatakiwa kuiga sauti na toni ya mwalimu au mfano uliowekwa<br>使用数字资源，例如专注于提高语言音调技能的应用程序或手机应用程序。<br><br>**Midia:** Tumia rasilimali za dijitali kama programu za simu za mkononi zinazolenga kuboresha ujuzi wa toni katika lugha | | | |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) 正确使用标点符号书写简单的文本（大写、小写、句号、逗号、叹号和问号）<br>Kutumia alama za uakifishaji katika kuandika maandishi sahili (Herufi kubwa, herufi ndogo, Kituo, mkato, alama ya kuuliza) | 说明和示例：带领学生详细解释并给出正确使用标点符号的示例，例如大写字母、小写字母、句号、省略号、问号和感叹号。解释每个标点符号在文字中的使用方式，并提供涉及这些标点符号的词语或句子的示例<br>**Maelezo na mifano:** Ongoza wanafunzi kwa kina na kutoa mifano ya matumizi sahihi ya alama za uakifishaji, kama vile herufi kubwa (大写字母), herufi ndogo (小写字母), kituo (句号), mkato (省略号), | 标点符号在书写简单文本中被正确使用了<br>Alama za uakifishaji zimetumika kwa usahihi katika kuandika maandishi sahili | 田字格、图片和实物<br>Tianzige, picha ya watu wakiwa wanatambulishana na vitu halisi | |

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | alama ya kuuliza (问号), na alama ya mshangao<br>(感叹号)Eleza jinsi kila alama inavyotumika katika maandishi na toa mifano ya kuandika maneno au sentensi zinazohusisha alama hizo<br>校对和修正：当学生提交他们的作品时，对他们的标点符号使用进行校对和修正。提供准确的反馈和指导，以帮助他们改进使用<br>**Mifano ya maandishi:** Toa mifano ya maandishi yenye alama za uakifishaji ili wanafunzi waweze kuzisoma na kuzoea matumizi yake | | | |

## 四年级 **Darasa la IV**

表**3**：**Jedwali 3:** 四年级的具体内容*Maudhui ya Darasa la IV*

| 主要能力<br>**Umahiri mkuu** | 具体能力<br>**Umahiri mahususi** | 学习活动<br>**Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法<br>**Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准<br>**Vigezo vya upimaji** | 教学资源<br>**Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量<br>**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 掌握基本汉语技能<br>Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kichina | 1.1 培养汉语声母、韵母和声调的音素意识并掌握发音<br>Kumudu ufahamu wa fonimu na matamshi ya awali, mwisho, toni na hanzi | (a) 听和发音只有韵母组成的音节<br>Kusikiliza na kutamka sauti zinazoundwa na irabu tu | 听后复述：引导学生流利地听和复述课文<br>**Kusikiliza na kurudia:** Ongoza wanafunzi kusikiliza na kurudia matini kwa ufasaha | 音节发出的声音能被正确地听到和发音<br>Sauti zinazoundwa na irabu tu zimesikilizwa na kutamkwa | 带字幕的文本、带字幕的录音机<br>Matini zenye irabu, na vinasa sauti vyenye irabu | 15 |
| | | (b) 听和写只有韵母组成的音节<br>Kusikiliza na kuandika sauti zinazoundwa na irabu tu | 听后书写：学生使用数字工具听写字母<br>**Kusikiliza na kuandika:** wanafunzi kusikiliza na kuandika irabu kwa kutumia zana za kidijitali | 由音节组成的声音能被听到和书写<br>Sauti zinazoundwa na irabu tu zimesikilizwa na kuandikwa | | |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量**Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) 识别只有音节组成的生词 Kubaini maneno yenye sauti zinazoundwa na irabu tu | 游戏：带领小组中的学生识别仅由音节组成的声音的单词 **Michezo:** Ongoza wanafunzi kwenye makundi madogo madogo kubaini maneno yenye sauti zinazoundwa na irabu tu | 仅由音节组成的声音的生词被流利地拼出 Maneno yenye sauti zinazoundwa na irabu tu yamebainishwa | | |
| | | (d) 书写三个到四个笔画内的汉字 Kuandika hanzi za kichina zenye vijenzi vitatu hadi vinne | 项目工作：带领小组中的学生识别仅由音节组成的声音的生词 **Kazi mradi:** Ongoza wanafunzi kwenye kazi mradi kwa kuandika hanzi zenye vijenzi vitatu hadi vinne | 三个到四个笔画内的汉字被写了 Hanzi za kichina zenye vijenzi vitatu hadi vinne zimeandikwa | | |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量 **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 能够联系单词与环境中的对象 Kuhusianisha maneno na vitu katika mazingira | (a) 使用新学到的单词识别在家庭环境中发现的对象的名称 Kubaini majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira ya nyumbani kwa kutumia maneno mapya yaliyoainishwa | 谜语游戏：我们可以使用谜语和引人入胜的故事作为激励学生学习中文的方式, 谜语将帮助他们发展词汇量，理解单词的意义，并提高他们正确运用语言的能力 **Kutengeneza mazingira ya kubuni:** Ongoza wanafunzi kubuni mazingira ya nyumbani na kubainisha majina ya vitu vinavyopatikana nyumbani | 在家庭环境中找到的对象的名称被正确定义 Majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira ya nyumbani yamebainishwa kwa kutumia maneno mapya | 照片/图片和实物 Picha na vitu halisi | 15 |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量 **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 挑战思维：创建一个单词列表，其中包含与其他单词具有相同或相似的音素或发音的单词。请学生发现这些相似的单词并解释它们的意义差异，要求他们描述自己听到或发音每个单词的方式，并将其与其他单词进行比较<br><br>**Bungua bongo:** Weka orodha ya maneno ambayo yana fonimu au matamshi sawa au yanafanana na maneno mengine, waulize wanafunzi kugundua maneno hayo yaliyofanana na kueleza jinsi tofauti zao zinavyotafsiriwa kwa maana, waombe wanafunzi kuzungumza jinsi wanavyosikia au kutamka kila neno na kulinganisha na neno lingine | | | |

| 主要能力 **Umahiri mkuu** | 具体能力 **Umahiri mahususi** | 学习活动 **Shughuli za ujifunzaji** | 建议的教学方法 **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 评估标准 **Vigezo vya upimaji** | 教学资源 **Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | 课时数量 **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
